2240 Weston Road, Unit # 1102
Toronto,ON M9N 1Y8
Canada

30th November 2016

Waziri/Katibu Mkuu

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
S.L.P 9132 Dar es Salaam
1 Mtaa wa Ardhi, 1147 Kivukoni Front

Mwenyekiti Wa Tume/ Katibu Mkuu

Tume Ya Kurekebisha Sheria

Haki House
8 Luthuli Road/P O Box 3580
Dar es Salaam Tanzania

Balozi zote za Tanzania Ulimwenguni

YAH: Maoni, ya Wanadiaspora Watanzania Duniani Katika Maboresho ya Sera Mpya na Sheria ya Ardhi 2016/17.

Baraza la Diaspora ya Watanzania Duniani (nje ya nchi) kwa kuzingatia maoni ya wana-diaspora wanaoishi nje (ughaibuni) walio katika makundi mawili, yaani watanzania ambao bado ni watanzania ila ukaazi wao upo katika nchi wanazoishi ughaibuni na watanzania ambao ni wazawa kwa mujibu wa sheria ya uraia, isipokuwa wamechukua uraia wa nchi wanazoishi ughaibuni hivyo kupoteza sifa za kuwa raia kwa mujibu wa sheria zilizopo ambazo tunaamini zinahitaji maboresho kama ambavyo serikali imekiri na kuahidi katika nyakati mbalimbali.

Hivyo basi kwa kupitia fursa hii ya kutoa maoni kuhusu sera mpya ya Ardhi nchini, Baraza letu limepata mapendekezo toka nchi 37 ambazo watanzania hawa wanaishi na kupata fikra, maoni na michango yao kama wadau kuhusu masuala muhimu katika maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi.

Masuala haya yapo katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, na marekebisho yake pamoja na Sera nyingine mbalimbali za Taifa, Mipango ya Maendeleo, uwekezaji, ajira, uhamiaji, Dira ya Taifa kuwa Tanzania ya Viwanda na MKUKUTA.

20. Occupation of Land by non-citizen restricted

(1) For avoidance of doubt, a non-citizen, except ***"kwa kuwa uraia wa Tanzania kimsingi ni (Jus Sanguinis - The rights of blood), ambapo mtu hupata uraia kutokana na uhusiano wa kidamu na wazazi wenye uraia wa Tanzania wa kuzaliwa, Hii ina maana kwamba, pamoja na mtu kuzaliwa Tanzania anatakiwa pia kuwa na mzazi ambaye ni raia wa kuzaliwa. Kwa kuzingatia Falsafa hii na kuzingatia usalama na uhifadhi wa Ardhi kwa manufaa ya Taifa tunapendekeza ndani ya sera na sheria ya ardhi itamke kumtambua raia wa kuzaliwa wa Tanzania aliyebadili, uraia na kuwa raia wa nchi nyingine, kwa hadhi maalum kumiliki ardhi kama Watanzania isipokuwa kwa wale wenye mlengo wa kuhatarisha usalama wa nchi au kuhujumu au kuwa na dhumuni la kujinufaisha kisiasa au kuwa na malengo ya kutumia fursa hiyo kwa malengo tofauti na dhumuni la sera na sheria yake***," shall not be allocated or granted land unless it is for investment purposes under the Tanzania Investment Act *(23).

Umuhimu wa maeneo ya mikakati, njia na mbinu ambazo zinapaswa kuzingatiwa na kuwepo katika Sera Mpya ya Taifa ya Ardhi ni ***ufuatialiaji na tathimini ya sera kufanyika mara kwa mara*** hii itasaidia kuondoa kero zinazojitokeza kutokana na mahitaji, mazingira na ushikilishwaji wa wadau tofauti kubadilika

2240 Weston Road, Unit # 1102
Toronto,ON M9N 1Y8
Canada

Pili Sheria za Ardhi kwenda na wakati na mahitaji halisi kwa kuzingatia mabadiliko katika jamii, bila kuathiri mila na desturi za mtanzania na tatu ni Elimu na taarifa kuhusu sera na sheria ya Ardhi nchini.

Manufaa kutokana na uwekezaji, Ardhi ikitolewa kwa uwekezaji mkubwa, wananchi wanufaike na uwekezaji huo kwa ardhi hiyo kupangishwa na mwekezaji na wananchi wapewe malipo kila mwaka kutokana na thamani ya ardhi inavyoongezeka kwa kuzingatia miaka ambayo mwekezaji ameomba kuwekeza, pia Wananchi wapewe hisa ya umiliki wa sehemu mradi husika na sehemu ya mapato yake ikatwe kodi na serikali ili kuboresha huduma za kijamii katika eneo husika kuliko ilivyo hivi sasa ambapo wawekezaji hutoa "peanuts" kwa jamii husika.

Ukomo wa umilikishaji wa ardhi

Utaratibu uliopo uendelee, na Rais wa Jamhuri aendelee kuwa mdhamini "Trustee" wa Ardhi yote ya Tanzania, na mamlaka ya kufuta umiliki kwa mujibu wa sharia iliyopo.

Best Market value

Valuation of assets at market price, Is not adequately reflected in the current market value, the Terms of sale should include clawback provisions in Order to fulfil the Government's or public body's Obligation to the taxpayer to obtain the best price...." failure to comply with the state aid rule, will mean that the subsidy is unlawful and may result in the benefit being recovered (with interest) from the recipient

Ulinzi wa maeneo maalum.

Utaratibu wa sasa, maeneo ya fukwe na visiwa yamewekewa masharti ya kuendelezwa na hivyo kutotumiwa au yanatumiwa kidogo.Utaratibu wa sasa uendelee, hivyo fukwe na visiwa visitolewe kwa waendelezaji, kwa sababu za kiusalama isipokuwa serikali yenyewe inaweza kuyaendeleza maeneo haya kwa maana kuwa chanzo cha mapato chini ya usimamizi na ulinzi wake.

Mgawanyo wa ardhi

Katika mpangilio wa utawala wa Ardhi wa sasa, mamlaka ya kugawa ardhi ndani ya kijiji yako mikononi mwa wananchi na viongozi wao katika kijiji. Hata hivyo ardhi kubwa inachukuliwa na watu kutoka mijini na kuna migogoro mingi ya ardhi, hii ni Dhahiri kuwa Usimamizi katika vijiji hawana utaalam, ufahamu, elimu na uwezo wa kutosha kuthaminisha ardhi na madhara yanayoweza kujitokeza, hivyo ardhi yote nchini irejeshwe chini ya usimamizi kamili wa Kamishna wa Ardhi na wataalam wake wilayani isipokuwa wapewe uwezo Zaidi wa vifaa na uwajibikaji wao uangaliwe kwa karibu na kwa umakini ili kutokuwa kero kwa wananchi wa eneo husika.

Hayo ndio maoni yetu. Tunaomba kuwasilisha.

Wako Watiifu,
Abraham S. Sangiwa - Interim Chairman - TDC Global
Kny: Kamati Maalum Ya Watanzania Waishio Nje (Diaspora Ya Watanzania Duniani)